East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 7, Issue 1, 2024
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Mapokeo ya Utenzi wa Mwana Kupona katika Upya wa Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'

*Gladys Kinara[1*], Dkt. Pamela Muhadia Yalwala Ngugi[1] na Dkt. Richard Makhanu Wafula[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100, Nairobi, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: glamoke@yahoo.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*11 Julai 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Utenzi, Mwana Kupona, Upya, Shaaban Robert, Utenzi wa Hati, Utenzi wa Adili.*

## IKISIRI

Makala hii inalenga kuchunguza mapokeo ya Utenzi wa Mwana Kupona katika upya wa tenzi za Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili' Robert (1967). Mapokeo yanaweza kuelezwa kama mila, desturi, fikra na hisia za kihistoria zinazohusu mtazamo sio tu wa yaliyopita zamani lakini pia uwepo wa mambo ya kihistoria na ya sasa kwa lengo la kuyapitisha kwa jamii (Sangi na wengine, 2012). Uchambuzi wa kazi hii umeegemezwa katika mihimili ya nadharia ya Bakhtin (1981) inayoshikilia kwamba lugha huwa na nguvu za Kani Kitovu na Kani Pewa. Kiwango cha Kani Kitovu huhusu nguvu za kisheria zinazotambulisha lugha. Hizi ni sheria za kisarufi na hazibadiliki. Katika muktadha wa fasihi, nguvu hizi zinawakilisha utamaduni wa jamii ambao daima unabaki kurithishwa na kufuatwa kama kanuni. Kiwango cha Kani Pewa nacho kinatokana na matumizi ya lugha katika jamii yanayobadilika kiwakati na yanatofautisha taaluma, tabaka na matumizi mengine ya lugha katika jamii. Nguvu za Kani Pewa zinajaribu kusukuma vipengele vya lugha kutoka katikati na kupelekea kuwa na wingi. Katika kiwango cha fasihi, nguvu za Kani Kitovu zinawakilisha utamaduni wa jamii ambao daima unabaki kurithishwa na kufuatwa kama kanuni. Kwa upande mwingine, kiwango cha Kani Pewa kinatokana na matumizi ya lugha katika jamii yanayobadilika kiwakati na yanayotofautisha taaluma, tabaka na matumizi mengine ya lugha katika jamii. Nguvu za Kani Pewa zinajaribu kusukuma vipengele vya lugha kutoka katikati na kupelekea kuwa na wingi. Katika kiwango cha fasihi, nguvu za Kani Pewa zinawakilisha upya na katika muktadha huu Utenzi wa Mwana Kupona katika tenzi za Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'. Utafiti ulikuwa wa kimaelezo na ulifanywa maktabani na nyanjani. Sampuli ya maktabani na nyanjani iliteuliwa kimakusudi. Maktabani, mtafiti alisoma kwa kina matini iliyochapishwa kwa lengo la kupata data ya msingi. Nyanjani, mtafiti alifanya mahojiano na majadiliano na wanajamii walioteuliwa katika kukusanya data. Data kutoka katika tenzi zilizoteuliwa, maandishi yaliyohusu utafiti, data ya nyanjani zilichambuliwa kulingana na lengo la makala haya na mihimili ya nadharia kwa lengo la kuonyesha namna mapokeo ya Utenzi wa Mwana Kupona yalivyobainika katika upya wa maandishi ya tenzi za Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na' Utenzi wa Adili'. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kwamba Shaaban

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043

Robert (1967) katika kuandika 'Utenzi wa Hati' na' Utenzi wa Adili' aliazima pakubwa kutoka katika Utenzi wa Mwana Kupona mbali na kuongeza upya kwa mujibu wa hali ya kijamii ya wakati wake.

**APA CITATION**

Kinara, G., Ngugi, P. M. Y. & Wafula, R. M. (2024). Mapokeo ya Utenzi wa Mwana Kupona katika Upya wa Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 319-331. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043.

**CHICAGO CITATION**

Kinara, Gladys, Pamela Muhadia Yalwala Ngugi and Richard Makhanu Wafula. 2024. "Mapokeo ya Utenzi wa Mwana Kupona katika Upya wa Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 319-331. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043

**HARVARD CITATION**

Kinara, G., Ngugi, P. M. Y. & Wafula, R. M. (2024) "Mapokeo ya Utenzi wa Mwana Kupona katika Upya wa Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 319-331. doi: 10.37284/jammk.7.1.2043

**IEEE CITATION**

G. Kinara, P. M. Y. Ngugi & R. M. Wafula "Mapokeo ya Utenzi wa Mwana Kupona katika Upya wa Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 319-331, Jul. 2024.

**MLA CITATION**

Kinara, Gladys, Pamela Muhadia Yalwala Ngugi & Richard Makhanu Wafula. "Mapokeo ya Utenzi wa Mwana Kupona katika Upya wa Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Jul. 2024, pp. 319-331, doi:10.37284/jammk.7.1.2043.

## UTANGULIZI

*Utenzi wa Mwana Kupona* ni utenzi maarufu na umeshughulikiwa na wataalam mbalimbali kufikia sasa. Tangu utenzi huu kutungwa mwaka wa 1858 kumekuwa na washairi mbalimbali ambao wametunga tenzi zinazoelekea kuwa kama mwangwi wa utenzi huo na yaelekea kuwa utafiti wa aina hiyo haujatiliwa maanani. Ili kuziba pengo hilo, uchanganuzi ulifanywa kwa kuzingatia tungo mahsusi zikiwemo *Utenzi wa Mwana Kupona* uliotungwa 1858 na kuchapishwa 1971 na Allen, J. W. T., 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili' katika Tawasifu ya Shaaban Robert, *Maisha Yangu na Baada Ya Miaka Hamsini* (1967). Makala hii ililenga kuchunguza mapokeo ya *Utenzi wa Mwana Kupona* katika upya wa Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili' kwa kuzingatia mapokeo ya *Utenzi wa Mwana Kupona* Allen (1971) katika tenzi za Shaaban 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'.

### Dhana ya Mapokeo na Upya

Wamitila (2003) anafafanua mapokeo kama kanuni na kaida zinazozingatiwa katika utanzu fulani. Kulingana naye, mapokeo ni kaida, desturi au fikra zinazozingatiwa katika utunzi wa tanzu mbalimbali za fasihi na hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Upya nao ni mabadiliko yanayotokea katika kazi ya fasihi kando na yale asilia katika mpwito wa wakati. Upya huu unaweza kutokea kwa njia na viwango anuwai. Unaweza kutokana na mwingiliano matini unaoleta mwangwi, mahusiano ya matini, wizi wa maandishi, usimilisho, utohozi wa kifasihi, uhamishaji wa fasihi au marekebisho ya kifasihi (Mdee, Njogu na Shafi, 2011).

Katika fasihi za Kiafrika zilizoandikwa kwa Kiingereza, dhana ya mapokeo na upya inajibainisha katika tanzu mbalimbali na kwa namna mbalimbali. Kwa mfano, riwaya ni utanzu mgeni katika bara la Afrika uliotokea katika karne ya ishirini. Utanzu huu ulifuata utanzu wa ushairi na tamthilia zilizotangulia kuchipuka. Ili kufanya utanzu huu kupokelewa katika mazingira mageni, wasanii wa riwaya walitegemea miundo ya Ulaya ya usanii wa riwaya pamoja na miundo asili ya masimulizi ya fasihi iliyozua mchanganyiko wa tenzi, ngano, hadithi, mighani, visasili na historia ya wanajamii katika riwaya ya leo (Kehinde, 2003). Mchanganyiko huu umefafanuliwa kikamilifu na Okwena (2019) kwa kutumia dhana

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043

ya umahuluti. Kulingana naye, umahuluti ni mchanganyiko wa mawazo na miundo tofauti katika kazi ya mwandishi. Aidha, umahuluti ni zao la maendeleo na njia ya utamaduni ambayo kwayo mwingiliano wa matukio hutukia. Kwa hivyo, riwaya za asili ziliazima kutoka katika umahuluti huu ili kufanya kazi hizi kupokelewa katika jamii kama utanzu uliokuwa ukichipuka.

Kwa mujibu wa Kehinde (2003), anwani ya riwaya ya Achebe (1994), '*Things Fall Apart'* imeazimwa kutoka katika shairi la W. B. Yeats '*The Second Coming'*. Achebe alichukua mstari mzima na kuufanya kichwa cha riwaya yake. Pia, msuko wa riwaya hiyo inayoelekea kushabihiana na utamaduni wa kitanzia wa ki-Aristotle inatokana na ukopaji wa riwaya ya Hardy (2015) '*Mayor of Casterbridge'*. Waaidha, tamthilia ya *The Gods are not to Blame* ya Rotimi 2011, ina mwingiliano na tamthilia ya Kigiriki ya *Mfalme Edipode*. Nayo tamthilia ya *Mfalme Edipode* imeazima motifu yake kutoka katika kazi za Homer ambapo miungu waliamua hatima za wahusika hata kabla kuzaliwa.

Katika fasihi ya Kiswahili, mapokeo na upya yamedhihirika katika uhusiano kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. Fasihi Andishi kwa kiasi kikubwa iliazima kutoka katika kazi za fasihi simulizi (Wamitila, 2003). Kwa hivyo, mapokeo yanakuwa kazi ya fasihi simulizi nayo fasihi andishi inakuwa upya. Katika muktadha wa makala haya, mapokeo ni utamaduni wa Waswahili kama unavyoonyeshwa na *Utenzi wa Mwana Kupona* nao upya ni mabadiliko yanayotokea katika kazi za sanaa zilizosimilishwa au zinazofanana kidogo na zilizochapishwa baada ya *Utenzi wa Mwana Kupona* kama vile tenzi za Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'.

## Suala la Utafiti

*Utenzi wa Mwana Kupona* ni utenzi maarufu na mkongwe na umeshughulikiwa na wataalam mbalimbali. Utenzi huu ulitungwa mwaka wa 1858. Kuanzia miaka ya 1890 utenzi huu ulianza kuchapishwa huko Ulaya katika hati ya Kirumi. Toleo la kwanza la *Utenzi wa Mwana Kupona* katika kipindi hiki ni lile la Alice Werner na William Hichens 1934 (Mulokozi, 1999). Tangu wakati huo, tenzi nyingine zimetungwa ambazo kwa njia moja au nyingine zinarindima mwangwi wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Hizi ni pamoja na Shaaban Robert (1967) katika 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'. Ni nadra kupata kazi zilizotafitiwa kuthibitisha mapokeo haya katika kazi za fasihi andishi ya Kiswahili. Ni katika muktadha huu ambapo makala haya yalilenga kuchunguza namna mapokeo ya *Utenzi wa Mwana Kupona* (Allen, 1971) yanavyobainika katika upya wa maandishi ya Robert (1967) ya 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'.

## YALIYOANDIKWA KUHUSU *UTENZI WA MWANA* KUPONA

Sehemu hii imeshughulikia uhakiki wa yaliyoandikwa kuhusu mada kwa lengo la kubaini pengo la makala husika. Sehemu ya kwanza imeshughulikia tahakiki za *Utenzi wa Mwana Kupona* na sehemu ya pili ilichunguza tahakiki za tenzi za Shaaban Robert (1967) katika 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'**.**

### Tafiti Kuhusu Utenzi wa Mwana Kupona.

Kuna tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu *Utenzi wa Mwana Kupona*. (Strobel, 1979, Njozi, 1990, Khatib, 1985, Biersteker, 1991, Swaleh, 1992;, Gibbe, 1995, na Wandera, 199). Tafiti za baadaye ambazo zimechambua *Utenzi wa Mwana Kupona* ni pamoja na Mulokozi (1999), Momanyi (2007), Beja na Mwinyifaki (2013), Timammy na Swaleh (2013) na Munyole (2017). Tafiti hizi zilitumia nadharia tofauti tofauti kwa kuzingatia malengo ya watafiti husika. Kazi hizi zote kuhusu *Utenzi wa Mwana Kupona* zilikuwa muhimu katika kubainisha pengo la makala haya ambayo yalilenga kuchunguza mapokeo ya *Utenzi wa Mwana Kupona* (1971) katika upya wa Shaaban Robert (1967) katika 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili' (1967).

### Tafiti Kuhusu tenzi za Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'.

Kuna tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'. Gakuo, (1996),

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043

Maina, (2005), Watuha, (2011), Gwakee na wenzake, (2017). Tafiti za wahakiki hao zilikuwa muhimu katika kuchangia uhakiki wa makala haya. Hata hivyo, tofauti na makala haya wahakiki hao walitumia nadharia tofauti tofauti mbali na kuangazia hoja tofauti katika uchambuzi wao. Makala haya yalilenga kuangazia mapokeo ya *Utenzi wa Mwana Kupona* katika upya wa maandishi ya Shaaban Robert kwa kurejelea 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili' (1967).

**Misingi ya Nadharia**

**Nadharia ya Bakhtin kuhusu Lugha**

Nadharia hii iliasisiwa na Mikhail Bakhtin ambaye alikuwa Mwanafalsafa wa Kirusi. Aliandika kazi zake katika miaka baada ya mapinduzi ya Urusi ya 1917. Kazi za Bakhtin ziliendelezwa na kusambazwa na baadhi ya wahakiki wakiwemo: Hirschkop na wenzake (2001), Holquist (2002) na Brandist (2002) miongoni mwa wengine. Kulingana na Bakhtin (1981), lugha inatawaliwa na kani za aina mbili: Kani Kitovu na Kani Pewa. Maneno haya yalibuniwa katika lugha ya Kirusi baadaye yalitafsiriwa katika lugha ya Kiingereza na kisha katika Kiswahili katika Kamusi ya Bayolojia, Fizikia na Kemia. Katika somo la Fizikia, Kani Kitovu: ni sehemu ya nguvu inayoelekezwa kwenye kitovu au katika mhimili mkuu wa mzunguko. Nguvu za Kani Pewa nazo ni kinyume cha nguvu za Kani Kitovu zinazovuta kwenda nje ya kitovu (Wamitila, 2003).

Bakhtin (1981) anasema, nguvu za Kani Kitovu zilifanya kazi kwa kuvuta vipengele vyote vya lugha na mbinu zake za ufasaha kuelekea katikati ili kutoa lugha moja iliyo sanifu au rasmi ambayo kila mmoja alizungumza na kuitumia. Nguvu hizo za Kani Kitovu zilikuwa kanuni zilozounganisha na kuleta kitu katikati. Katika muktadha wa makala hii, nguvu za Kani Kitovu ziliwakilisha utamaduni wa Waswahili kama unavyoelezwa na *Utenzi wa Mwana Kupona* wakati huo wa karne ya 18 na 19.

Kwa upande mwingine, nguvu za Kani Pewa zilijaribu kusukuma vipengele vya lugha kutoka katikati na kupelekea kuwa na wingi wa lugha au vijilugha katika jamii. Kwa kuwa nguvu hizi zilivuta kwenda nje zilidengua na ziliweka katika tabaka na hivyo basi zilienda kinyume na kanuni za Kani Kitovu. Bakhtin anadai kuwa, lugha haikugawanywa katika lahaja tu, bali katika lugha iliyoashiria taaluma, utanzu, kizazi, kikundi na umri miongoni mwa mambo mengine. Katika muktadha wa makala hii, matini ambayo iliathiriwa na nguvu za Kani Pewa ziliendelea kubadilikabadilika kila wakati. Mabadiliko haya yaliwakilisha upya ambao ulitokea katika kazi za sanaa zilizosimilishwa au zinazofanana kidogo na zilizochapishwa baada ya *Utenzi wa Mwana Kupona*.

Nguvu kati ya Kani Kitovu na Kani Pewa ziliwasilisha mabadiliko ya lugha na zilihakikisha kuwa daima mabadiliko hayo yalibakia kushindana. Nadharia hii ya Bakhtin iliongoza uhakiki wa makala hii ambayo ililenga kuchunguza mapokeo ya *Utenzi wa Mwana Kupona* katika upya wa Shaaban Robert hasa katika 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo. Utafiti ulifanywa maktabani na nyanjani. Maktabani, mtafiti alisoma kwa kina matini iliyochapishwa kwa lengo la kupata data ya msingi. Nyanjani, mtafiti alifanya mahojiano na majadiliano na wanajamii. Sampuli ya maktabani na nyanjani iliteuliwa kimakusudi. Maktabani, mtafiti alisoma vitabu, tahakiki, tasnifu kwa lengo la kupata pengo la utafiti na data ya msingi. Nyanjani, mtafiti aliteua wasailiwa saba ambao waliteuliwa kutokana na umri wao, jinsia na kiwango cha elimu katika jamii ya Lamu. Mtafiti alitumia mwongozo wa maswali na mijadala kama nyenzo kuu katika ukusanyaji wa data ya upili. Data ya nyanjani na maktabani iliainishwa kulingana na namna mapokeo ya *Utenzi wa Mwana Kupona* yalivyobainika katika upya wa Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'. Data kutoka katika tenzi zilizoteuliwa pamoja na maandishi yaliyohusu utafiti zilichambuliwa kulingana na lengo la makala hii kwa kujikita

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043

katika mihimili ya nadharia kwa lengo la kuonyesha namna mapokeo ya *Utenzi wa Mwana Kupona* yanavyobainika katika upya wa maandishi ya Shaaban Robert.

## UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA MATOKEO

Sehemu hii itashughulikia uchanganuzi wa matokeo katika *Utenzi wa Mwana Kupona* Allen (1971) na Robert (1967) katika 'Utenzi wa Hati' na' Utenzi wa Adili'. Sehemu ya Kwanza itashughulikia mapokeo ya *Utenzi wa Mwana Kupona* katika tenzi za Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na' Utenzi wa Adili'nayo sehemu ya pili itashughulikia upya wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'.

### Mapokeo ya Utenzi wa Mwana Kupona Katika 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'

Sehemu hii itashughulikia mapokeo ya *Utenzi wa Mwana Kupona* katika tenzi za Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na' Utenzi wa Adili'. Mapokeo yanayojadiliwa ni pamoja na dhamira ya watunzi, mafundisho ya dini, heshima, adabu na wema, bidii, heshima na utangamano wa wanajamii kwa jumla.

### Dhamira ya Watunzi

Mapokeo ya Mwana Kupona yanabainika kutokana na dhamira ya Robert. Katika tawasifu yake ya *Maisha Yangu na Baada Ya Miaka Hamsini* (1967). Robert alioa mke wake wa kwanza Amina na walifanikiwa kupata watoto wawili: mmoja alikuwa ni mwana, wa pili alikuwa binti. Binti alikuwa kifungua mimba na mwana alikuwa kitinda mimba. Baadaye Amina alifariki. Robert alisikitishwa mno kwa ukosefu wa malezi ya mama ya watoto wao. Badala yake ilimpasa ajaribu kutenda jambo jingine bora aliloweza mahali pa malezi ya mama yao. Basi aliandika tenzi mbili, mmoja kwa kila mtoto (Robert, 1967). Robert alikusudia kujaza pengo la malezi kwa kutunga 'Utenzi wa Hati' kwa ajili ya kutoa maelekezo ya mzazi kwa binti ambaye mamake hakuwepo. Aidha, alitaka kumpa bintiye hati ambayo ingemfaa mbali na kumpamba kwa wema katika dunia.

Miktadha ya utunzi ya Robert na Mwana Kupona ilikuwa tofauti. Robert alilazimika kutunga tenzi baada ya kufiwa na mkewe na kumwachia pengo la malezi ya watoto wao. Mwana Kupona naye alitunga tenzi kwa kuhofia kuwa afya yake ilikuwa imedorora na alihisi kuwa hangeishi kwa muda mrefu (Allen, 1971:-2). Mapokeo ya Mwana Kupona yanabainika kutokana na lengo la utunzi ambalo lilikuwa suala la malezi. Watunzi hawa wote waliwatakia watoto wao makuzi mema kama toleo la nguvu za Kani Kitovu. Bakhtin (1981) anasema kuwa, nguvu za Kani Kitovu zinapovuta vitu vyote kwenda kati, zinaoanisha vitu hivyo na kwa hivyo zinasanifisha na kurasimisha kwa kuviwekea kanuni. Katika muktadha wa fasihi, yaliyorasimishwa yanakuwa mapokeo yanayostahili kufuatwa kama sheria. Katika muktadha huu, Robert anafuata mfano wa Mwana Kupona kwa kutunga utenzi ili kumuusia bintiye mwanzo kama alivyofanya Mwana Kupona na pili kutoa maelekezo ya maisha kwa bintiye.

### Mafundisho ya Dini

Katika 'Utenzi wa Hati', Robert (1967) anamuusia binti yake Hati kuzingatia suala la dini. Anamwomba kushikamana na ibada kwa kuwa itamfaidi wakati dunia itakapokwisha. Anaendelea kumwambia kuwa dini ni amali ya roho kama vile mavazi yaliyo ya mwilini. Anamuasa ashike dini ataepuka uroho na anasa za dunia. Vilevile, katika 'Utenzi wa Adili' Robert (1967), anamwambia mwanawe Adili kuwa ni muhimu kuishi maisha ya kumwogopa Mwenyezi Mungu. Aidha, Robert anamuusia Adili kumcha Mungu kwa kuwa ndiye aliyeumba ulimwengu juu akaweka mbingu na nyota ziangaze (*Utenzi wa Adili*, Robert,1967:- ubeti wa 10).

Wakishadidia haya, Gwakee na wenzake (2017), wanabainisha namna Robert alivyoyakumbatia masuala ya kidini katika dini ya Kiislamu. Suala la dini linabainisha namna nguvu za Kani Kitovu zinavyovuta kwenda kati. Nguvu hizi zinabainisha namna 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043

wa Adili' zinavyoelekea kufanana na *Utenzi wa Mwana Kupona* hasa zinaposhughulikia suala la dini kama toleo la nguvu za Kani Kitovu. Katika muktadha huu, suala la dini linaonekana kurasimishwa na kuwa kanuni muhimu katika tungo hizi. Kanuni hii inakuwa utamaduni unaofuatwa na wanajamii kama sehemu ya maisha yao.

Nyanjani, wahojiwa walishadidia haya kwa kusema kuwa, dini ilikuwa sehemu ya utamaduni wao na hawangeweza kutofautisha dini na utamaduni. Wahojiwa walidai kuwa, walipozaliwa waliwakuta wazazi wao wameizingatia dini na hawakuona sababu ya kupotoka. Bakhtin (1981) anasema kuwa, nguvu za Kani Kitovu zimerasimishwa na kusanifishwa kwa hivyo suala la dini linabainika katika tenzi zote na ni muhimu katika malezi ya wanajamii wote wanaofuata mafundisho ya Kiislamu.

**Heshima, Adabu na Wema**

Robert (1967) anamuusia bintiye Hati katika 'Utenzi wa Hati' kuheshimu baba na mama, watu wazima na rika lake. Kulingana naye, ukosefu wa adabu ni jambo la aibu sana kwa hivyo ajaribu kujiepusha nalo. Gwakee na wenzake (2017) wakihakiki 'Utenzi wa Adili' wanasema kuwa, Robert alimuusia, Adili kuwaheshimu wazazi wake na akiweza awatendee kila kilichochema. Robert anahisi kuwa, suala la heshima ni muhimu kama alivyoona Mwana Kupona katika *Utenzi wa Mwana Kupona* Alllen 1971:- ubeti wa 13.

Wahojiwa nyanjani walithibitisha kuwa, suala la adabu lilisisitizwa katika malezi ya wanajamii mbali na kufundishwa katika madrasa. Wanajamii walihitaji kuwaheshimu wanajamii wengine. Kwa mfano, ilikuwa adabu kwa mtoto kumuamkua mtu anayemzidi kwa kusema 'Shikamoo'. Huo ulikuwa utamaduni wa jamii. Heshima hiyo ilistahili kuzingatiwa katika jamii nzima kama sehemu ya mafundisho ya dini. Hii inatokana na sababu kuwa, haya ni mapokeo ya jamii na hayapatikani tu katika dini ya Kiislamu bali pia katika dini nyinginezo na jamii zote. Kwa hivyo, kulingana na Bakhtin (1981), Kani Kitovu inabainisha mapokeo ya jamii ambayo yamerasimishwa na kusanifishwa na hivyo kuwa utamaduni ambao unastahili kufuatwa. Mawazo haya yanonyesha makubaliano katika tenzi hizi na kuhakikisha kuwa kazi hizi zinastahili kufuatwa kama mapokeo ya wanajamii wote bila kubagua jinsia, umri wala wakati na hivyo kuleta wiano katika tenzi hizi katika muktadha wa Kani Kitovu.

**Kuwa na Bidii**

Katika *Utenzi wa Adili*, Robert (1967) anamkanya Adili dhidi ya uvivu akisema kuwa ajiepushe na uvivu kwa kuwa uvivu huzaa umaskini. Robert anamwomba Adili afanye kazi yake vizuri. Robert (1967) anamuusia Hati katika 'Utenzi wa Hati' kujitegemea kwa kuwa ni ngao dhidi ya ukiwa. Kulingana naye, iwapo mumewe anaweza kufariki mbele yake naye abakie mjane anaweza kujitegemea. Mawazo ya Robert yanaoana na Mwana Kupona kwa kuwa Mwana Kupona pia alimkanya bintiye dhidi ya uzembe. Mwana Kupona anamuomba bintiye asiwe mzembe, afanye kazi zote zikiwemo kufagia na kuosha choo bila dharau.

Nyanjani, wahojiwa walithibitisha kuwa, utamaduni wa jamii yao haukuhimiza uzembe kwa njia yoyote ile. Mwanamume alipokwenda kazini kama vile kuvua samaki, wanawake walihitaji kujishughulisha kwa namna mbalimbali. Wengine walikuwa wakipika vitumbua, samosa, wengine walishiriki katika biashara, wengine ususi, wengine walifanya majukumu ya malezi kule nyumbani almuradi kila mmoja alishiriki katika kufanikisha jamii. Mawazo haya yanaonyesha wiano katika tenzi hizi kama toleo la nguvu za Kani Kitovu kwa kuwa bidii ni sehemu ya maadili ya jamii na kwa hivyo ni mapokeo yanayostahili kurithishwa jamii kutoka kizazi hadi kizazi kama sehemu ya nguvu za Kani Kitovu.

**Kuzingatia Usafi**

Katika 'Utenzi wa Hati', Robert (1967) anamuusia Hati kuhakikisha kuwa nyumba yake ni nadhifu kwa kuhakikisha kuwa anafagia uchafu ili kila mdudu dhaifu asipate pa kukaa. Mawazo ya Robert (keshatajwa) yanaoyesha ulinganifu na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043

yale ya Mwana Kupona ya kuzingatia usafi wa mwili na nyumba pamoja na kuosha choo (Allen, 1971, ubeti, 37).

Katika muktadha wa tenzi hizi, Kani Kitovu zinavuta kwenda kati kwa kurasimisha na kusanifisha hivyo kubainisha muumano uliopo katika tenzi hizi. Suala la usafi linabainika kuwa la kimsingi hivyo kuonyesha utamaduni wa wanajamii ambao unapokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

**Utangamano na Wanajamii kwa Jumla.**

Katika 'Utenzi wa Hati', Robert (1967) anazungumzia suala la utangamano na heshima. Anasema ni bora kumheshimu kila mtu kwa sababu hujui ni nani atakayekufaa. Aidha, katika mawazo ya kutangamana na wafalme, Robert (1967) katika 'Utenzi wa Adili', anasema ingekuwa bora kuheshima kila mmoja katika jamii bila kubagua jinsia mradi kila mmoja alifanya wajibu wake. Katika 'Utenzi wa Hati' Robert (keshatajwa), anamuusia bintiye kuwajali wanajamii wote wanyonge na wenye vyeo na kumsisitizia kuwa hayo ni maadili na hivyo basi ndiyo mapokeo. Mawazo haya yanaonyesha uwiano uliopo kati ya tenzi hizi na *Utenzi wa Mwana Kupona*. Hii inatokana na sababu kuwa, Robert aliwausia Hati na Adili suala la heshima katika kutangamana. Suala la utangamano na heshima kwa kila mwanajamii linaonekana katika tenzi za Robert na Mwana Kupona hivyo kuwa kanuni katika jamii kama toleo la nguvu za Kani Kitovu.

Sehemu hii ilishughulikia mapokeo ya *Utenzi wa Mwana Kupona* katika upya wa tenzi za Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na' Utenzi wa Adili'. Mapokeo yaliyobainika ni kama dhamira ya watunzi, mafundisho ya dini, heshima, adabu na wema, kuwa na bidii, kuzingatia usafi na utangamano na wanajamii na hivyo kuonyesha namna nguvu za Kani Kitovu zinavyofanya kazi katika kuimarisha mapokeo ya jamii. Sehemu itakayofuata itashughulikia upya wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika tenzi mbili za Robert (1967): 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'

**Upya wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'**

Sehemu hii itashughulikia upya wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na' Utenzi wa Adili'. Upya huo ni pamoja na jinsia ya watunzi na mazingira ya utunzi, idadi na vichwa vya tenzi, suala la ufisadi, umuhimu wa elimu, mapenzi na ushirikiano katika ndoa, maendeleo katika maisha, umuhimu wa msamaha, kuweka siri na kutimiza ahadi.

**Jinsia ya Watunzi na Mazingira ya Utunzi**

Mwana Kupona binti Mshamu Nabhany naye alizaliwa Pate mwaka 1810. Baadaye alihamia Lamu baada ya kukumbwa na maafa mengi ya jamaa yake. Akiwa Lamu, alitunga utenzi wake mwaka 1858 (Mulokozi na Sengo, 1995). Shaaban Robert alizaliwa tarehe 1/1/1909 katika kijiji cha Vibambani, kata ya Machui huko Tanga, Tanzania. Wazazi wake wote wawili walikuwa wa ukoo wa Mganga wa kabila la Kiyao. Hata hivyo, Robert hakujiita Myao kabisa, bali alikuwa mmojawapo wa wachache ambao daima walijiita Waswahili. Robert alikuwa yatima akiwa na umri wa miaka tisa wakati baba yake mzazi alipofariki mwaka 1918. Robert alihamishwa Dar es Salaam akalelewa na babu yake aliyekuwa akiitwa Abubakari. Huko ndiko alikopata mwanga wa elimu ya shule katika shule ya Kichwele ambayo sasa inaitwa Uhuru Mchanganyiko. Alisoma hapo kuanzia mwaka wa 1922 hadi 1926 na kufaulu mitihani yake vizuri (Robert, 1967 na Mulokozi, 2003).

Watunzi hawa walitoka katika maeneo tofauti Kijiografia jambo ambalo liliathiri lahaja waliyotumia. Kwa mfano, Mwana Kupona alitumia lahaja ya Kiamu naye Shaaban Robert akatumia Kiunguja (Kiswahili Sanifu). Mwana Kupona aliishi katika mazingira yaliyoathiriwa na Waarabu. Kwa hivyo, elimu ya wakati wake ilisisitiza masuala ya dini. Robert naye alizaliwa katika kipindi cha majilio ya Wakoloni; Wajerumani na Waingereza. Nyakati hizo elimu ya Kimagharibi ilikwisha anzishwa na Shaaban Robert alikuwa mmoja wa wale waliopata elimu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043

hiyo. Vilevile alipata ajira baada ya kumaliza masomo yake mwaka wa 1926. Kazini, mbali na kupandishwa cheo, alipata uhamisho mara kadha wa kadha. Mazingira haya tofauti yaliathiri mwonoulimwengu wa watunzi hawa na hivyo kubainisha nguvu za Kani Pewa.

Mwana kupona alitunga *Utenzi wa Mwana Kupona* mwaka wa 1858. Utenzi huu ulitungiwa binti yake Mwana Hashima bint Shee Mataka. Inasemekana kuwa, Mwana Kupona alitunga utenzi huu akiwa anaugua maradhi ya tumbo la uzazi. Alihisi kuwa asingepona. Hivyo akaamua kutunga utenzi ili uwe ni wosia kwa binti yake ambaye angebaki bila maelekezo ya mama (Muokozi, 1999). Jamii ya Waswahili ilimpa mama nafasi kubwa katika malezi ya watoto (Mbaabu, 1985). Mwana Kupona alipohisi kuwa alikuwa mgonjwa, aliona bora amwelekeze bintiye kwa kutumia utenzi. Nyakati tofauti walizotunga tenzi hizi zinabainisha kiwango kingine cha Kani Pewa kutokana na nyakati za utunzi mbali na kuwa watunzi hawa walikuwa wa jinsia tofauti.

Waaidha, Shaaban Robert alitunga tenzi zake miaka mia moja baada ya Mwana Kupona (Mulokozi, 1999). Miaka mia moja ni muda mrefu na jamii ilikuwa imebadilika kisiasa, kijamii na kiuchumi. Kwa sababu hiyo, mazingira ya wakati wake yalimwathiri kutokana na elimu aliyopata na tajriba iliyotokana na kutangamana na wanajamii mbalimbali. Robert alijua kuwa, watoto wake walikuwa tofauti na majukumu yao yalikuwa tofauti hasa katika muktadha wa mabadiliko ya kijamii. Hivyo basi alihitajika kutunga tenzi mbili na kubainisha majukumu ya kila mmoja katika tenzi hizi.

## Idadi na Vichwa vya Tenzi

Shaaban Robert aliwatungia watoto wake tenzi mbili baada ya mke wake kuaga dunia (Robert, 1967). ‘Utenzi wa Hati’ ulitungiwa binti Mwanjaa nao ‘Utenzi wa Adili’ ukatungiwa mwana Selemani. Aidha, tenzi hizi zilikuwa na ujumbe tofauti kwa kila mtoto kwa kuwa zililenga watoto wa jinsia tofauti.

Mwana Kupona alitunga utenzi mmoja kwa ajili ya binti yake mwana Hashima binti Shee Mataka (Mulokozi, 1999). Ijapokuwa Mwana Kupona alitunga utenzi mmoja kwa ajili ya bintiye, yeye kama mama alikuwa na wajibu mkubwa katika malezi ya watoto ama wa kike au kiume (Mbaabu, 1985). Kwa mfano, katika *Utenzi wa Mwana Kupona*, baadhi ya mambo anayoyasema yanaweza kuzingatiwa pia na mtoto wa kiume. Mwana Kupona anapomuusia bintiye kuwa asikie maneno kwa kuwa kiumbe ni radhi tano ndipo apate amani ya akhera na dunia, mawaidha haya pia yanaweza kumfaa mtoto wa kiume kwa kuwa radhi nyingine zinakaririwa katika mafundisho ya dini yanayowafaa waumini wa dini ya Kiislamu. Kwa mfano, radhi ya kwanza ni ya Mungu na Mtumewe, kisha baba na mama na ya tano ni ya mumewe. Mvulana anastahili kuyajua haya kwa kuwa yamekaririwa pia katika Kurani; mamlaka yake juu ya mwanamke yanabainika. Mvulana anaweza kusoma na akajua majukumu yake atakapokuwa mume; yeye anastahili kutoa radhi kwa mke wake. Japo mvulana hakutungiwa utenzi, jukumu la malezi katika jamii ya Waswahili lilikuwa la mama hadi mtoto alipofika miaka sita hadi saba ambapo alipelekwa madrasa (Mbaabu, 1985).

Kulingana na Mohammed (2016), mtoto wa kike akishabaleghe hufundishwa na akina mama naye mtoto wa kiume hufundishwa na akina baba. Kwa hivyo, jukumu la kumlea binti lilikuwa kubwa kwa Robert hata akalazimika kumtungia bintiye utenzi kwa lengo la kumuelekeza. Mwana Kupona alitekeleza jukumu lake la malezi hasa kuhusiana na bintiye. Huenda ndiyo maana alitunga utenzi mmoja naye Robert akatunga tenzi mbili. Aidha, tenzi hizi zilikuwa na vichwa tofauti. Kwa hivyo, tofauti iliyopo katika tenzi hizi zinaonyesha namna nguvu za Kani Pewa zinavyofanya kazi kwa kuleta tofauti katika tenzi hizi hasa Robert anapolazimika kumtungia binti utenzi ilhali jukumu hili lilikuwa la akina mama.

## Suala la Ufisadi

Robert (1967) anamuusia bintiye katika ‘Utenzi wa Hati’ kuambaa ufisadi. Kulingana naye, ufisadi hutia mtu doa. Robert anamwomba bintiye

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043

asiingize ufisadi katika maisha yake ili asije akajiharibia maisha. Kulingana na Bakhtin (1981), Kani Pewa huleta usambazaji kwa kuonyesha sauti mbalimbali. Kani hizi zinahimiza tofauti na wingi sauti. Katika muktadha huu usambazaji huu unatupa upya unaotokana na maudhui mapya ya ufisadi aliyoangazia Robert. Majilio ya wageni yalileta ufisadi suala ambalo lilimuudhi Robert. Kwa hivyo, suala la ufisadi linakuwa upya tofauti na yale aliyoangazia Mwana Kupona kama toleo la Kani Pewa.

**Umuhimu wa Elimu**

Katika 'Utenzi wa Hati' Robert', (1967) anamuusia bintiye kupata elimu. Kulingana naye, elimu itamfanya kuwa na taaluma. Pia, anaweza kutenganisha halali na haramu. Robert anamuusia bintiye ajifunze elimu rasmi kwa kuwa ni kama nuru inayoangaza jangwani katika maisha ya mwanadamu. Anaongezea kuwa, elimu ni kitu kizuri kwa kuwa akiwa nayo atapata fahari kwa kuwa itamshauri. Robert anamuusia bintiye mawaidha ya wakati wake kwa kuwa yeye alifaidi elimu rasmi ya wakati wake. Kama ilivyoelezwa awali kuwa Robert alipata mwanga wa elimu katika shule ya Kichwele ambayo sasa inaitwa Uhuru Mchanganyiko. Alisoma hapo kuanzia mwaka wa 1922 hadi 1926 na kufaulu mitihani yake vizuri (Shaaban, 1978: vi, Mulokozi, 2003).

Elimu ya wakati huo ilikusudia kukabiliana na ulimwengu wa wakati wake tofauti na wa Mwana Kupona. Elimu ya wakati wa Mwana Kupona ilitolewa na kungwi kwa ajili ya kumsaidia anayeipokea kuitunza nyumba yake. Bali na kumpa maarifa, ilihusu kumjua Rabuka kwa hivyo, nguvu za Kani Pewa zinabainisha upya katika 'Utenzi wa Hati' kutokana na maudhui aliyoendeleza Robert ambayo yaliangazia elimu ya kimagharibi ya wakati wake. Robert (1967) pia anamuusia Adili katika 'Utenzi wa Adili' kupata elimu. Kulingana na Robert, elimu ina nafasi maalum kwa yule anayeelewa. Robert anamsisitizia Adili kuwa hatapata ufanisi akikosa elimu.

Kwa mujibu wa mtunzi, ni vigumu kwa mtu asiyekuwa na akili na macho kuona nafasi ambazo ni finyu. Kwake Robert, aliye na elimu ana ufunguo wa maisha katika kupata nafasi za kazi. Anamkanya Adili kutofanyia elimu mchezo kwa kuwa elimu ndiyo nguzo ya maisha. Anaongezea kuwa, elimu ina mwanga maalum. Kulingana na Robert, maisha yasiyokuwa na elimu hayafai mwanadamu kwa sababu siku zijazo kuna mambo mengi magumu. Kwa mujibu wa mtunzi, ingawa dunia ni pana, ni vigumu kwa mtu asiyekuwa na akili na macho ya kuona nafasi ambazo ni finyu. Anamkanya Adili kufanyia mzozo onyo analopewa kwa kuwa mtu aonywapo, huwa nguzo ambayo kwayo mafunzo huegemea.

Maudhui haya ya elimu yanadhihirisha Kani Pewa inafanya kazi kwa kuonyesha tofauti katika mazingira ya wakati wake Robert hasa ikizingatiwa kuwa alitunga tenzi hizi baada ya Wamishenari na Wakoloni kuja katika nchi za Afrika Mashariki na kuleta elimu ya Magharibi. Allen anatoa maelezo kumhusu Robert katika utangulizi wa *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1978: Vi) kwa kusema:

> *Alielimishwa Dar-es –Salaam toka mwaka wa 1922 hata mwaka wa 1926, akawa mtu wa pili katika wanafunzi kumi na mmoja waliofaulu mtihani wao na kupewa shahada ya kutoka chuoni ya 'School Leaving Certificate.*

Masomo haya yaliathiri utunzi wake kwa kuwa yeye alifaidi elimu hii. Basi alipokuwa akimuusia mwanawe Adili hakuwa na budi kusisitiza haja ya kuzingatia elimu kwa kuwa wakati wake ulihitaji mtu aliyeelimika kuajiriwa serikalini. Kando na kipindi hicho ambapo wasichana wengi hawakuenda shule, Shaaban anamuasa bintiye akumbatie elimu na apate taaluma kinyume na hali ilivyokuwa. Maudhui haya ya elimu yanabainisha upya katika tenzi za Robert (1967) 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili' kama toleo la nguvu za Kani Pewa zinazovuta kwenda nje na kuonyesha tofauti na *Utenzi wa Mwana Kupona.*

**Mapenzi na Ushirikiano katika Ndoa.**

Ndoa ni uhusiano uliopo kati ya mke na mume baada ya taratibu maalum zilizokubalika na jamii kwa lengo la kuanzisha familia. Taasisi ya ndoa ni

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043

muhimu sana kama anavyoashiria Robert. Robert (1967) anamuusia Adili katika 'Utenzi wa Adili' kuwa, akioa mke amwonesha mapenzi wala asimfanyie machachari na vishindo. Anamuusia kumheshimu mke wake kama mama mzaa watoto kama yeye alivyozaliwa. Anamwambia awapende watoto wake na awatendee awezalo ili liwafae baadaye *(Robert*, 1967, ubeti, 59).

Mawazo haya ya Robert yanabainisha upya unaotokana nguvu za Kani Pewa zinazoleta upya. Kwa sababu yanaonyesha kuwa, ufanisi katika ndoa hautamtegemea tu mke; bali pia ushirikiano mkubwa kati ya mke na mume. Kwa hivyo, Adili kama mume pia ana wajibu katika ndoa kwa kuonyesha mapenzi kwa mke na wanawe. Mawazo yanayoonyesha tofauti na *Utenzi wa Mwana Kupona.*

Vilevile, Robert (1967) anamuusia bintiye Hati katika "Utenzi wa Hati" kuwa, wasishindane na mume wala wasinuniane. Hati anaambiwa, ajitahidi wapatane kwa kuwa hayo ndiyo maisha ya ndoa. Anaombwa kufanya kila awezalo kulikubali la mume ili ndoa yao ifanikiwa. Hata hivyo, Robert anaongezea kwa kumwambia bintiye kuwa, hatakuwa na hatia kukataa maneno ya mumewe iwapo si halali.

Katika utenzi huu Robert anawausia watoto wake wote. Mawaidha anayompa Hati yangeweza kuwafaidi yeye na nduguye Adili. Ndio maana anatumia kiambishi 'M'. Kuna tofauti kubwa katika toni na maneno katika wito wa Robert kwa bintiye na *Utenzi wa Mwana Kupona* ambaye anamuusia binti pekee. Robert anawausia Hati na Adili ushirikiano katika ndoa kwa kuwa anafahamu ufanisi katika ndoa unatokana na ushirikiano kati ya mke na mume. Robert anazungumzia "ninyi wawili" wala si binti pekee. Anasema "Msishindane","Msinuniane", "Mpatane" wala si "Usishindane" mahali ambapo kiambishi awali "M" kinaashiria wingi na "U" umoja.

Falsafa iliyoongoza mwelekeo huu na uchaguzi wa maneno si tu tofauti na ule wa *Utenzi wa Mwana Kupona* bali pia unakinzana na falsafa ya ushairi wa kimapokeo. Maafikiano katika ndoa ni kitu ambacho hakikuwahi kusikika katika ulimwengu wa Mwana Kupona kwa kuwa mume ndiye alikuwa na mamlaka. Ni mwanamke aliyestahili kujinyenyekeza kwa mume wake na kula na kupumua kwa mapenzi yake mume. Momanyi (1998) akishadidia haya anasema kuwa, mausio ya Robert katika beti hizi ni yale ya ushirikiano. Maneno kama 'Msishindane', 'Msinuniane', 'Mpatane', 'Ijengeni' yanaashiria ushirikiano kati ya mke na mume tofauti na sauti ya Mwana Kupona iliyoashiria maelekezo kwa bintiye pekee.

Naye Robert anaelekeza binti yake katika ushirikiano huu kwa kupuuza maneno ya mumewe iwapo si halali katika mishororo miwili katika ubeti wa 35. Robert anamshauri bintiye kupuuza matendo ya mumewe iwapo matendo hayo si halali. Kwa mujibu wa Momanyi (1998), maelekezo kama haya yanatokana na uhalisi wa dini ya Kiislamu ambayo inapinga maovu yanayoshurutishwa na mtu mwingine. Kwa sababu kila binadamu, mume au mke atahukumiwa kulingana na matendo yake binafsi bali sio kupitia kwa kauli za binadamu mwingine. Kwa upande mwingine, Ndulute (1987) anashadidia mawazo haya anaposema kuwa, Robert anamuusia bintiye kumkataza mumewe mapenzi na heshima zake iwapo anahisi kuwa amedhalilishwa anaposema, "Ila lisilo halali kukataa si hatia". Mawazo ya Robert (1967) yanabainisha Kani Pewa ikifanya kazi kwa kuwa tofauti na yale ya Mwana Kupona ambaye anamwambia bintiye kufanya lolote kutimiza anayotaka mume. Jambo linaloonyesha kuwa mawazo ya Robert yalikuwa tofauti kutokana na mabadiliko ya nyakati alizoishi kama toleo la nguvu za Kani Pewa.

**Maendeleo katika Maisha**

Robert (1967) katika "Utenzi wa Hati' anamuusia bintiye Hati azingatie maendeleo. Maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kielimu yalikuwa masuala muhimu wakati katika jamii. Wake kwa waume hawakuwa na budi kushiriki shughuli ambazo zingeleta maendeleo kwa vyovyote vile. Vilevile, anamuusia asingojee bahati kwa kuwa ana wajibu wa kujishughulisha kwa vitendo.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043

Anamtahadharisha kwa kusema kuwa watu wengi wamekosa kujiendeleza kimaisha kwa kutojituma na wakati mwingine kupoteza bahati maishani (Robert, 1967, ubeti, 45). Mawazo ya Shaaban yanahimiza maendeleo katika jamii katika vipengele mbalimbali vya maisha. Jamii ya wakati huo ilikuwa ikiangazia maendeleo. Sio tu ya kielimu, bali pia ya kijamii na kisiasa. Maendeleo haya hayangefikiwa iwapo wanajamii wangelaza damu. Ilimlazimu kila mmoja kujituma. Kwa hivyo, mawazo haya yanabainisha upya kama toleo la nguvu za Kani Pewa za lugha kwa kuwa tofauti na yale aliyokuwa akiusiwa Mwana Kupona.

**Umuhimu wa Msamaha**

Robert (1967) anamuusia Adili katika' Utenzi wa Adili' kuomba msamaha. Kulingana naye, anapomwomba mkewe msamaha watafaidi wote. Anaongezea kuwa, msamaha ni kitulizo cha moyo kwa kuwa huwapa furaha wote wanaohusika, anayetoa na anayepewa (Robert, 1967, ubeti, 60). Mawazo haya yanaonyesha tofauti na yale Mwana Kupona alimuusia bintiye katika *Utenzi wa Mwana Kupona*. Mwana Kupona anamwambia bintiye aketi na mume wake kwa adabu wala asimtie ghadhabu. Mumewe akinena asimjibu, ajitahidi kunyamaza. Anaongezea kuwa aende naye kwa imani wala asimnyime analotaka. Anamwomba kutoshindana naye kwa kuwa ushindani huumiza (Allen, 1971, ubeti, 28).

Mwana Kupona anaonyesha kuwa, binti anastahili kujinyenyekeza kwa mumewe ili ndoa ifaulu. Lakini, Shabaan anaona suala la ndoa kama linalohitaji ushirikiano kutoka pande zote ili lifaulu ndio maana tofauti na Mwana Kupona, anamuusia Adili kutomfanyia mkewe kelele labda mkewe aanzishe. Hayo yanapotokea, anaweza kuomba msamaha kwa kuwa msamaha ni kama kitulizo cha moyo; huwafanya wote wanaohusika kufurahi. Kani Pewa inabainika kutokana na mawazo tofauti aliyoangazia Robert. Nia yake ilikuwa kuonyesha kuwa ndoa ni asasi iliyohitaji ushirikiano na unyenyekevu palipohitajika. Robert anaibua mawazo mapya ya msamaha kama suluhisho katika kufanikisha ndoa.

**Kuweka Siri na Kutimiza Ahadi**

Robert (1967) anamuusia Adili katika 'Utenzi wa Adili' kutofichua siri zake kwa watu asiowajua na kutowaamini. Kulingana na Robert, kuna mambo yanayostahili kujulikana na watu na kuna yale yanayohitaji kufichwa. Siri za nyumbani husitiriwa na wahusika wote ili kufanikisha ndoa. Mawazo haya yanabainisha upya kwa kuwa yanaelekea kuwa tofauti na yale aliyousiwa Mwana Kupona. Mwanaume ana wajibu wa kuwa mwaminifu. Siri inakuwa sehemu muhimu katika uaminifu wa ndoa. Si mwanamke tu anayestahili kuwa mwaminifu.

Waaidha, Robert (1967) anamkumbusha Adili umuhimu wa kutimiza ahadi. Anamwambia kuwa, akiweka ahadi ajitahidi kuitimiza. Kulingana na Robert, kutimiza ahadi ni heshima. Kabla ya kutoa ahadi, mtu anastahili kuipima ndipo aitamke. Pia, anaongezea kuwa ahadi haibadilishwi ila iwe batili. Iwapo ni halali ni vyema kuitimiza (Robert, 1967, ubeti, 78).

Kulingana na Wamitila (2003), Kani Kitovu na Kani Pewa ni dhana zinazohusishwa na Mikhail Bakhtin aliyezitumia kuelezea mvuto wa kutoka nje ya kitovu fulani. Kani hizi kwa mujibu wa Bakhtin (1981), zinapatikana katika lugha. Kwa mfano, kuna mvuto kuelekea kwenye usawishaji wa lugha unaoshikiliwa na kundi fulani na wakati uo huo mvuto wa kiusambazaji ili kuonyesha sauti mbalimbali. Bakhtin anaamini kuwa, kuna tanzu fulani ambazo zina mwelekeo wa Kani Kitovu yaani kumvuta msomaji kwenye ukubalifu fulani na nyingine ambazo zina Kani Pewa au zinazohimiza tofauti na wingi sauti. Masuala ya kuweka siri na kutimiza ahadi yaliyotokana na nguvu za Kani Pewa za lugha zilizoonekana kuwa tofauti na masuala aliyoshughulikia Mwana Kupona katika Utenzi wa Mwana Kupona.

Sehemu hii ilishughulikia upya wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili'. Upya ulibainika katika jinsia ya watunzi na mazingira ya utunzi, idadi na vichwa vya tenzi, suala la ufisadi, umuhimu wa elimu, mapenzi na ushirikiano katika ndoa, maendeleo katika maisha, umuhimu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

wa msamaha, kuweka siri na kutimiza ahadi. Sehemu itakayofuata itatoa hitimisho.

## HITIMISHO

Makala haya yalilenga kuchunguza mapokeo ya *Utenzi wa Mwana Kupona* katika upya wa Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili' kwa kuongozwa na nadharia ya Bakhtin kuhusu lugha. Ilibainika kuwa mapokeo ya *Utenzi wa Mwana Kupona* yalibainika katika upya wa tenzi za Shaaban Robert ikiwemo: dhamira ya watunzi, mafundisho ya dini, heshima adabu na wema, kuwa na bidii na kuzingatia usafi ni mambo yaliyoonekana kuwa mapokeo ya jamii na yalizingatiwa katika jamii ya watunzi hawa kama toleo la nguvu za Kani Kitovu. Kwa upande mwingine, kuna mambo ambayo yalionekana kuwa tofauti na kuleta upya katika tenzi husika. Haya ni kama jinsia ya watunzi, idadi ya tenzi ambayo pia ilibainika kuwa Shaaban alitunga tenzi mbili kwa ajili ya watoto wake tofauti, suala la ufisadi na umuhimu wa elimu. Vilevile, Robert aliangazia mapenzi na ushirikiano katika ndoa, maendeleo katika maisha, umuhimu wa msamaha, kuweka siri na kutimiza ahadi. Haya yalibainika kuwa mapya katika tenzi za Shaaban Robert: 'Utenzi wa Hati' na 'Utenzi wa Adili' kama toleo la Kani Pewa. Upya ambao huenda ulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo muktadha, ukinzani au falsafa ya watunzi kutokana na athari ya wageni kutoka nje ya Afrika.

## MAREJELEO

Achebe, C. (1994). *Things Fall Apart*. New York: Anchor Books.

Allen, J. W. T. (1971). *Tendi*. Nairobi: Heinemann.

Bakhtin, M. (1981). *Discourse in the Novel. Modern Literary Theory*. 4th Edition. London: Routledge.

Beja, S. K. na Mwinyifaki, A. (2013). 'Iktibasi' katika *Tenzi za Mwanakupona* na *Al-Inkishafi*. *Kioo cha Lugha, 11*(1), 30-46. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Biersteker, A. (1991). "Language, Poetry and Power: A Reconstruction of 'Utendi wa Mwana Kupona.' In Harrow, K. W. (Ed.), '*Faces of Islam in African Literature'*. pp 37-58. London: James Currey.

El-Maawy, A. A. A. (2011). *Jawabu la Mwana Kupona*. Dar es Saalam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Dar es Salaam.

Gakuo, J. K. (1996). Fani Katika Utenzi wa Vita vya Uhuru. *Tasnifu ya Uzamili. Eldoret: Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).*

Gibbe, A. G. (1995). Inkishafi: Uhakiki wa Kidayakronia. *Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Moi. Eldoret. (Haijachapishwa).*

Gwakee, J., Timammy, R. na Mogambi, H. (2017). 'A comparative Analysis of Virtue-Based Content for Youth in Two Epics in Swahili: Siraji and Adili'. *International Journal of Languages and Linguistics*. 4, 4.

Hardy, T. (2015). *The Mayor of Casterbridge*. Tustin: Xist Publishing.

Hirschkop, K. & Shepherd, D. (Eds.). (2001). *Bakhtin and cultural theory*. Oxford: Oxford University Press.

Holquist, M. (2002). *Dialogism: Bakhtin and His World*. London: Routledge.

Kehinde, A. (2003). 'Intertextuality and Contemporary African Novel'. In *Nordic Journal of African Studies*. 12(3): 372-386. Uppsala: The Nordic Africa Institute.

Khatib, M. S. (1985). '*Utenzi wa Mwana Kupona*' katika *Mulika*. Na. 17: 46-52. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Maina, V. (2005). Nafasi ya Mwanamke Katika Tenzi Mbili za Shaaban Robert. *Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).*

Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili*. Nairobi: Kenya Publishing and Book Marketing Co. LTD.

Mdee, J. S., Njogu, K. & Shafi, A. (2011). *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja*. Nairobi: Longhorn.

Mohamed, F. A. (2016). Kuchunguza Mila na Desturi za Mwanamke wa Visiwani Pamoja na Fani katika Tenzi za *Howani na Mwana Kukuwa. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa).*

Momanyi, C. (1998). Usawiri wa Mwanamke Muislamu Katika Jamii ya Waswahili kama Inavyobainika Katika Ushairi wa Kiswahili.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043

*Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).*

Momanyi, C. (2007). ‘Patriachal Symbolic Order: The Syllables of Power as Accentuated in Waswahili Poetry.’ In *The Journal of Pan African Studies*, 1, 8.

Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar-es-salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. & Sengo, T. S. (1995). *History of Kiswahili Poetry, AD 1000-2000: a Report.* Institute of Kiswahili Research. University of Dar es Salaam

Munyole, S. D. (2017). Usomaji na Ufasiri Sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Chuo kikuu cha Kenyatta. *Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa)*.

Ndulute, C. L. (1987). Shaaban Robert's Poetic Landscape: From Ethnicism to Nationalism' *Kiswahili*. Vol. 54, No. 1/2, pp. 92-116. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Njozi, H. M. (1990). *Utendi wa Mwana Kupona* and Reception Aesthetics. *Kiswahili*, *57*, 55-67.

Okwena, S. (2019). Umahuluti wa Miundo Katika Tamthilia za Ebrahim Hussein. *Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).*

Robert, S. (1967). *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Dar es Salaam: Thomas Nelson and Sons Ltd.

Sangi, M. K. et. al. (2012). ‘T. S. Eliot and the Concept of Literary Tradition and the Importance of Allusions’. *International Journal of Science and Research*.1, I, 3. India: American Association for the Advancement of science.

Strobel, M. (1979). *Muslim Women in Mombasa. 1890-1975*. New Haven and London: Yale University Press.

Swaleh A. (1992). Maudhui Katika *Utenzi wa Mwana Kupona*. *Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).*

Timammy, R. na Swaleh, A. (2013). ‘A Thematic Analysis of Utendi wa Mwana Kupona: A Swahili Islamic Perspective’ In *Journal of Education and Practice*. 4, 28.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Limited.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications.

Wandera, S. P. (1996). “Usawiri wa Mwana Kupona Katika Ushairi wa Kiswahili: 1800-1900; Uhalisi au Ugandamizwaji? *Tasnifu ya Uzamili; Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa).*

Watuha, A. I. (2011). Maudhui ya Waadhi katika Utenzi wa Adili. *Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)*.